fondation BOTNAR INNOVEX

TANGA CITY COUNCIL

10 MAY 2022

OFFICE OF THE CITY DIRECTOR REGISTRY OFFICE

# TANGAZO LA KAZI

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA KWA KUSHIRIKIANA NA MDAU WA MAENDELEO –FONDATION BOTNAR KUPITIA SHIRIKA LA INNOVEX NA ESFR-MNCH ANATANGAZA NAFASI ZA KAZI ZA WATOA HUDUMA WA SEKTA YA AFYA WENYE SIFA KAMA IFUATAVYO**

## 1. MTEKNOLOJIA MACHO II (NAFASI 3) TGHS B

### SIFA ZA KUAJIRIWA

Mwenye Stashahada (Diploma) ya Sayansi katika fani ya macho kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na Mabaraza ya Taaluma pale inapohusika

### KAZI NA MAJUKUMU

1. Atafanya kazi za huduma za afya ya msingi ya macho.
2. Kufanya uchunguzi na kutibu magonjwa ya macho
3. Kupanga na kuratibu utaratibu wa kuhudumia wagonjwa wa macho nje ya kituo (Outreach clinic).
4. Kubuni mbinu za kuboresha huduma za macho katika eneo lake la kazi.
5. Kutafsiri takwimu na taarifa zilizokusanywa na kuzifanyia kazi
6. Kutoa ushauri nasaha (provider initiated for conselling and testing for HIV/AIDS).
7. Kuchonga miwani.
8. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.



TANGA CITY COUNCIL

10 MAY 2022

## 2. *MTEKNOLOJIA MSAIDIZI MAABARA ( NAFASI 13) TGHS A*

### SIFA ZA KUAJIRIWA

Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha Nne wenye cheti cha miaka miwili katika fani ya maabara kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza yao pale inapohusika.

### KAZI NA MAJUKUMU

(i) Kuandaa vitendanishi (reagents) vya kufanyia vipimo vya Maabara.
(ii) Kufanya kazi za awali sampuli zinazoletwa maabara
(iii) Kukusanya damu kutoka kwa wagonjwa na watu wanaojitolea
(iv) Kurekodi matokeo ya vipimo kwenye regista
(v) Kutayarisha vifaa vya kazi.
(vi) Kuhifadhi kwa mujibu wa taratibu sampuli zote zinazohitaji kuhifadhiwa baada ya uchunguzi.
(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

## 3. *MTEKNOLOJIA WASAIDIZI DAWA (NAFASI 4) TGHS A*

### SIFA ZA KUAJIRIWA

Mwenye Stashahada (Diploma) katika fani ya Dawa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

### KAZI NA MAJUKUMU

(i) Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.
(ii) Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi
(iii) Kuchanganya dawa
(iv) Kuhifadhi dawa na vifaa tiba
(v) Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa
(vi) Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi
(vii) Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.
(viii) Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospitali
(ix) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
(x) Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi



CITY COUNCIL
10 MAY 2022
OFFICE OF THE CITY DIRECTOR

(xi) Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.
(xii) Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chnini yake
(xiii) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
(xiv) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

## 4. *TABIBU II (NAFASI 14) TGHS B*

### SIFA ZA KUAJIRIWA III

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha Nne/Sita wenye Stashahada ya Tabibu/ ya muda wa miaka 3 kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

### KAZI NA MAJUKUMU

(i) Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi
(ii) Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida
(iii) Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo
(iv) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi
(v) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii
(vi) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
(vii) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji
(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

## 5. *MUUGUZI DARAJA LA II – (NAFASI 45) TGHS A*

### SIFA ZA KUAJIRIWA

Kuajiriwa mwenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

### KAZI NA MAJUKUMU

(i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali Na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
(ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi.

TANGA CITY COUNCIL
10 MAY 2022
OFFICE OF THE CITY DIRECTOR
REGISTRY OFFICE

(iii) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa Kazi.
(iv) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
(v) Kutoa ushauri nasaha
(vi) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
(vii) Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
(viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
(ix) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
(x) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

## 6. *MTEKNOLOJIA (RADIOLOJIA) DARAJA II – TGHS B (NAFASI 2)*

**SIFA ZA KUAJIRIWA**

Mwenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika fani ya Radiografa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

**KAZI NA MAJUKUMU**

(i) Kuwapima wagonjwa wanaolekezwa kwenye eneo lake la kazi
(ii) Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi.
(iii) Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality).
(iv) Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa.
(v) Kusimamia watumishi walio chini yake
(vi) Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya na kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
(vii) Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization).
(viii) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
(ix) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

10 MAY 2022

## MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45.
2. Maombi yambatanishwe na vivuli vya vyeti, picha moja ya passport size iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya mwombaji na namba ya simu.
3. Juu ya bahasha iandikwe kazi aliyoomba.
4. Transcript na provisional results hazitapokelewa.
5. Aidha kazi hii ni za mkataba wa miezi 6 tu.
6. ***Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/05/2022.***
7. Maombi yote yatumwe kwa:

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji,
S.L.P. 178,
**Tanga.**

Sipora Liana
**MKURUGENZI WA JIJI**
**TANGA**
MKURUGENZI WA JIJI
TANGA

Tangazo hili limetolewa na:
Ofisi ya Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji,
S.L.P. 178,
**Tanga.**

TANGA CITY COUNCIL
10 MAY 2022